

HABARI LEO UK 17.

Mifugo itaua hifadhi-Waitara

Na Veronica Mheta, Iringa

BODI ya Wadhamini ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), imetembelea Hifadhi ya Taifa Ruaha mkoani Iringa kujionea athari za uvamizi wa mifugo katika eneo la Bonde la Ihefu.

Wakiwa katika hifadhi walishuhudia mifugo zaidi ya 200,000 ikiwa ndani ya hifadhi.

Akizungumza jana katika hifadhi hiyo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Tanapa, Jenerali George Waitara alisema wamejionea uvamizi mkubwa wa mifugo ndani ya Hifadhi ya Taifa Ruaha hali inayohatarisha usalama wa hifadhi hiyo.

"Ikumbukwe hifadhi hizi ni mali yetu sote Watanzania na ni sehemu

ya uchumi wa Tanzania, wakati mifugo ni mali ya mtu mmoja mmoja. Hivyo ni jukumu letu kulinda hifadhi ambayo ni ya Watanzania wote kwa faida ya sasa na ya baadaye," alisema.

Aidha, Jenerali Waitara aliongeza kuwa mifugo itakuwa chanzo cha kufa kwa hifadhi nchini, kwani inaua mifumo ya ikolojia na kuhatarisha kutoweka kwa wanyama na mimea.

"Hivyo ni muhimu hifadhi hizi zikalindwa kufa na kuona, ili ziendelee kunufaisha taifa na kizazi kijacho," alisema.

Awali, akiwasilisha taarifa ya Hifadhi kwa Bodi, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Godwell Meing'ataki alisema walifanya operesheni kwa siku mbili na kufanikiwa kukamata mifugo zaidi ya 1,900 katika eneo hilo

la Ihefu na itaendelea kwa siku 10 zaidi kuanzia Septemba 13 hadi 23, mwaka huu.

Naye Profesa Wineaster Anderson ambaye ni mmoja wa wajumbe wa bodi hiyo, alisema Tanapa ina wajibu mkubwa wa kulinda maliasili zilizomo hifadhini kwa faida ya Watanzania wote.

"Tuna wajibu mkubwa katika taifa hili ya kulinda maliasili hizi pamoja na miradi ya kimkakati kama bwawa la kuzalisha umeme la Mwalimu Nyerere, ambalo linategemea maji kutoka vyanzo vilivyomo hifadhini Ruaha.

"Kiasi kikubwa cha fedha kimekwishatumika kujenga bwawa hilo na wananchi wana mategemeo makubwa ya kunufaika nalo,"

alisema. Naye Mjumbe mwingine wa bodi, Kamishna wa Polisi, Nsato Marijani, alisisitiza kuongeza nguvu katika kufanya doria na kuendeleza operesheni ya kuwaondoa wavamizi wote katika eneo la hifadhi hiyo.

Kamishna wa Uhifadhi wa Tanapa, William Mwakilema aliishukuru bodi ya wadhamini kwa kutembelea Hifadhi ya Taifa Ruaha, kujionea changamoto kubwa ya uvamizi wa mifugo ambayo ni tishio kwa uhifadhi nchini.

Alisema endapo hapatakua na juhudi madhubuti na za dhati za kudhibiti mifugo, itasababisha kufa kwa hifadhi hizo ambazo ni tunu kwa taifa na ambazo zinaingizia pato taifa, sifa na fahari ndani na nje ya nchi.